



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Tuesday, 10th March, 2026

Third Assembly – Fifth Session
TWELFTH SITTING

*[The County Assembly met at 2:31p.m at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]*

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Have your seats Members. Yes, Clerk confirm if there is quorum?

[Quorum confirmed]

Yes, Clerk next order please?

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

STUDY VISIT BY STUDENTS AND TEACHERS OF KINGWEDE GIRLS SECONDARY SCHOOL

Good afternoon, Honourable Members. I am pleased to acknowledge and warmly welcome the students and Teachers from Kingwede Girls Secondary School, who have joined us this afternoon and they include;

1. Martha Atieno
2. Mwanahamisi Suleiman
3. Elizabeth Mlongo
4. Namnyaka Sadina
5. Agnes Sendeu
6. Happiness Tuamini
7. Rose Nyavula
8. Jamila Abuu
9. Umazi Charo
10. Faith Katini
11. Hellen Jonson
12. Mwanamkuu Opreh
13. Amina Meselemani
14. Amina Pakia

15. Roda Tsuma
 16. Esha Rajab
 17. Furaha Ngome
 18. Amina Kalitu
 19. Fatuma Bwengo
 20. Feddis Taura
 21. Ajra Rengwa
 22. Mwanahamisi Ndila
 23. Aziza Said
 24. Saumu Kwekwe
 25. Jackline Menza
 26. Husna Bakari
 27. Anita Dama
 28. Karen Harison Ruwa
 29. Hadija Sharbaidi
 30. Hadija Bakari
 31. Jackline Woki
 32. Elizabeth Khamayo
 33. Zaitun Jaffar
 34. Zaitun Juma
 35. Lori Salome
 36. Agnes Khasunga
 37. Rehema Wakesho
 38. Hadija Koja
 39. Angel Happiness
 40. Mwaka Bakari
 41. Mwanajuma Jumanne
 42. Umi Abdalla
 43. Bintihamisi Rashid
 44. Fahima Alfani
 45. Doria Masuud.
- Accompanied by their Teachers;
46. Mr. Oginga Nuri
 47. Mrs. Halima Mercy
 48. Mr. Francis Odhiambo

It is always a great honor to host young minds eager to learn about the working of the County Assembly and the democratic processes that guide Governance in Mombasa, your presence here today, is a testament to your curiosity, ambitions and dedication to education. We hope that this visit inspires you to take an active interest in leadership saving responsibilities and community service. On behalf of the entire Assembly, we wish you a faithful, enlightening experience. *Karibuni sana* and I will let Honourable Athman Mwamwiri the Majority Leader to also welcome the students.

The Leader of Majority Party (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, let me take this opportunity to welcome the students from Kingwede Girls. Mr. Speaker, Kingwede Girls is in Ramisi Ward in Kwale County, specifically Msambweni Sub-County so we are thrilled to have the students today here with us. As the Leader of the majority, I'm honoured

to host them Mr. Speaker; the County Assembly is a space for them to explore, learn and share their thoughts and voices so that after this, they can make this great Country of Kenya a place to be and proud for their citizens. Mr. Speaker, maybe for their guidance and the teachers can assist them, the laws which govern the County Assemblies and the devolution in Kenya include the Constitution of Kenya specifically Article 174 to Article 200. Mr. Speaker, also they can learn much about the Devolution in the County Government Acts of 2012, Intergovernmental Relations Act of 2012 and the Public Finance Management Act of 2012 that is where Mr. Speaker, the whole issue of Devolution, County Governments and the County Assemblies are enriched Mr. Speaker. Thank you Mr. Speaker *na karibuni sana katika Bunge la Mombasa*.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you the Majority Leader and I will also let a namesake because we have Mwaka Bakari in the House. Honourable Mwaka Bakari please welcome the students.

Hon. Mwaka Bakari: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii. Mwanzo nataka kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mwezi huu mtukufu wa Ramadhan uliojaa neema na baraka tele, karibuni sana wanafunzi Kingwede Girls kutoka Kwale Kaunti. Karibuni sana pia vilevile ninafurahi sana kusikia kuna Honourable Mwaka Bakari hata mimi pia ni Mwaka Bakari:

[Applause]

Naomba asimame si nimuone!

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Mwaka Bakari, please communicate with the Speaker?

Hon. Mwaka Bakari: Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, ninaomba mwanafunzi anayeitwa Mwaka Bakari aweze kunipungia mkono ili tumuone Mheshimiwa kule juu.

[The student stood up and waved]

Ahsante sana Mheshimiwa Mwaka Bakari, *I wish you all the best*. Hata wewe utakuwa Mheshimiwa Mwaka Bakari pengine Kaunti ya Kwale ama Kaunti ya Mombasa. Mungu awabariki. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Okay. Thank you. Thank you Honourable Mwaka Bakari Mwaludonda. Yes, Clerk. Next order please?

BILL

THE MOMBASA COUNTY SUPPLEMENTARY APPROPRIATION BILL, 2026

SECOND READING

Yes, Honourable Kibwana Swaleh Baya.

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 3*

Hon. Kibwana Swaleh: Thank you Mr. Speaker. Honourable Speaker, allow me before I move my Motion to recognize the students as well as the teachers from Kingwede which is in Kwale and I have learnt from the Leader of Majority that is from Ramisi. I do not know whether which Ward is that! Is it constituency? Ramisi Ward Mr. Speaker. Honourable Speaker, mine is that you encourage the students to concentrate on their studies so at least they will make their future bright and as leaders we should also protect the child... girl child Speaker so at least they manouvre and complete their studies so I want to give a big thanks to the teachers as well as the principal who is not around that this is a place to learn about devolution since that is our backbone in our County. Honourable Speaker, I stand here to move a Motion that is; Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

That the Mombasa County Supplementary Appropriation Bill, 2026 be now read for a second time.

Honourable Speaker, allow me to ask one of my Member for budget and finance Honourable who is my Deputy to second for me. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): The Vice Chair.

Hon. Noor: I take this opportunity first of all to welcome the students the girls from King...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Hamida, second the Motion then you'll have time to...

Hon. Noor: I do second the Motion.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you.

Hon. Noor: So, I can welcome the students?

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): I give I will give you time to welcome the students. I propose a question that the Motion by Honourable Kibwana Swaleh Baya as moved be debated in this House?

*[Question put and agreed to]
[Consultations]*

Thank you. I have engaged the Table Clerk so I will repeat the question. Honourable Members, I propose a question that the Motion as moved be read a second time?

*[Question put and agreed to]
[Loud consultations]*

Yes, Members it's on the floor of that House. Honourable Kibwana?

Hon. Kibwana Swaleh: Thank you Honourable Speaker. Honourable Speaker, mine is just to say that this is a supplementary budget which to us is very critical so that uh both the County Government as well as the County Assembly can work and I think we will discuss a lot. There are a lot of projects that need this the passage of this supplementary so to be taken by the County government, so mine is just to ask my colleagues to give maximum support to this Supplementary so that at least we can pass it and then be able to utilize the funds that are in this supplementary budget. Thank you, Honourable Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Kibwana. Yes, Honourable Hamida. You can now as well welcome the students using your time.

Hon. Noor: Thank you, Mr. Speaker I stand again to welcome the students and I do support the Motion Honourable Honour because as we know we need the Supplementary Budget we can do our businesses as well as the County Executive and County Assembly so that we can finish our business for this term and I do support the Motion. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Thank you. Yes, Honourable Jactone Madialo?

Hon. Madialo: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii. Pia na mimi ningependa kuchukua fursa hii kukaribisha walimu na wanafunzi kutoka Shule ya Kingwede kutoka Kaunti ya Lamu, karibuni sana...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): It is Kwale.

Hon. Madialo: ...Kwale.

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Thank you.

Hon. Madialo: Ahsanteni sana kutoka Kaunti ya Kwale karibuni sana. Mheshimiwa Spika pia mimi ningependa kuchukua fursa hii kuunga mkono kwa dhati Hoja hii ambapo imeletwa na Mheshimiwa Kibwana ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ili hii Supplementary Budget ni vizuri tukapate kuunga mkono na mimi kama Mheshimiwa kutoka Wadi ya Mikindani ninaiunga mkono kwa dhati kwa sababu katika Bajeti hii pesa imewekwa tumeweka pesa ya kujenga hospitali Level 4 pale Mikindani na pia katika Bajeti hii tumeweka pesa ya kujenga barabara kilomita moja ambayo inatoka Mikindani kuelekea sehemu za Allidina na pia kuna hospitali ndogo ambapo kupitia kwa Bajeti hii itajengwa pale Kibarani kwa sababu hiyo mimi naunga mkono kwa dhati. Ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Maryam Baimu?

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii kwanza ningependa kuwakaribisha walimu na wanafunzi wa shule ya Kingwede Girls Secondary School karibuni sana Bunge muweze kusoma mawili matatu yale yanayofanyika katika Mabunge yetu ya Kenya kwa ujumla, kitu nitazidi tu kutia msisitizo ni kwamba mtu yeyote ama mwanafunzi yeyote kuweza kufanikiwa katika maisha yake lazima mwanzo atie bidii kwa masomo yake. Pili awe ni mtu anayependa kusoma, tatu aweze kuwa na *discipline* na ukiwa na ile *ambition* ama ari ya ku

excel basi *I believe what a man can do a woman can do better* na warembo wangu mnaona hapa Bungeni tuko na wa mama kadhaa hapa ambao wanawakilisha kule Wadi zao. Kwa hivyo imani yangu kama vile Mheshimiwa Mwenza ameongea Mwaka yeye ni Mheshimiwa na yuko mtoto jina lake pale hata la baba kwa hiyo imani yangu hata nyinyi nyote *take that initiative* mfanye bidii ili wengine wenu wale wanapenda mambo na siasa siku nyengine waweze kuwa katika Bunge zetu. Pili, Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono Mswada huu kwa sababu kusema ukweli Mheshimiwa Spika kazi zozote kufanyika katika Wadi zetu ni lazima kuwe na pesa kwa hivyo imani yangu vile vitu ambavyo vimewekwa kwa Bajeti tutakapokuwa tumepitisha hii Supplementary basi *In Shaa Allah* kazi mashinani zitaonekana. Nimesimama kuunga mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Ibrahim Omondi?

Hon. Omondi: Mr. Speaker thank you for the opportunity, first of all I would like to join my fellow colleagues to dearly welcome our students from Kingwede Girls, Kwale County that you are highly welcomed. Honourable Speaker, am very impressed that this month we have had a trend I can say a trend whereby we have had school girls visiting in this Hon. House consecutively, am very impressed that girls have got the passion to learn especially now that we embrace the CBC curriculum whereby the students can see they always say Mr. Speaker seeing is believing so by then seeing what you are doing I am sure that in future they will be able to put it in practical. I also like to give them one educational quote just to advice, encourage and motivate them Mr. Speaker I would like encourage the students that everyone can rise above their circumstances and achieve their successes if they are dedicated to what they do. Number two do not judge yourself by how many successes you have made but judge yourself on how many sometimes you have failed down and rose again. Thank you, Mr. Speaker, I join fellow Members to support the Motion on the Supplementary Bill. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Benard Ogutu?

Hon. Ogutu: Ahsante sana Mheshimiwa kwa nafasi hii pia niungane na wenzangu kuwakaribisha wanafunzi ambao wamekuja kusoma mahali hapa. Mheshimiwa Spika Hoja hii ambayo iko mbele yetu ni Hoja muhimu sana manake maendeleo ya Wadi zetu zinaandamana na pesa nafikiri tumekaa kwa muda mrefu sana bila kupata maendeleo kwa sababu hii Supplementary ilikuwa haijaletwa na tunaomba punde ikiletwa hizo pesa ziweze kuonekana zikifanya kazi kule mashinani Mheshimiwa Spika. Ahsante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Abdul Hamid?

Hon. Mohammed Hamid: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwanza ningelipenda kuwakaribisha wanafunzi kutoka Kwale hii ni dalili na ishara ya kuwa sisi sote ni wamoja na ni Wapwani karibuni sana musome tunayoyafanya hapa Mombasa. Pili, nimesimama kuunga mkono Hoja ilioko leo ya *Supplementary*, kusomwa kwa mara ya pili lakini kama vile wenzangu walivyotangulia kusema pesa tunapitisha tunapenda kuziona zikifanya kazi mashinani. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes, Honourable Hamisi Nyota?

Hon. Hamisi Nyota: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity I stand to support the second reading of the Bill as earlier mentioned by my colleagues we want to see development progress in this County and the only way we can ensure this county prospers in development is to ensure this House passes such essential Bills so we hope and believe by that it is going to propel the future development of this County. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Mbelle Patrick?

Hon. Mbelle: Shukran Mheshimiwa Spika kwanza nikaribishe dada zetu kutoka Kigwede Girls Mheshimiwa Spika hawa ni wasichana wa nyumbani nina watu wangu washasoma kule nisingetaka kusema kama wiki iliyopita...

[Laughter]

Lakini nina dada zangu wanasoma Kigwede Girls na ni shule nzuri nishaenda kuwatembelea upande ule nikapeleka chapati wakati huo siku hizo za nyuma, kwa hivyo najua Kigwede Girls ni shule nzuri na nawatakia kila la heri katika masomo yenu nawaombea Mwenyezi Mungu katika masomo yenu pia nyinyi mupite na siku moja aidha mukaa maskani kama hizi ndani ya Bunge ama Mwenyezi Mungu awabariki yale munayotaka katika maisha yenu yaweze kutimia kulingana na uwezo ambao atakao kua amewapa. Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono hoja ambayo hii ambayo inaipa Serikali ya kaunti uwezo kutumia fedha katika *Supplementary Budget*. Mheshimiwa Spika ninauunga mkono kwa sababu ninatambua ya kwamba maendeleo hayawezi kufanyika bila pesa na hakuna kuchimba ama kujenga kunawezekana bila ya kua na shilingi ya kununua simiti ama kununua chuma, kwa hivyo Mheshimiwa Spika tunaipa uwezo na nguvu Serikali ya kaunti ikiongozwa na Mheshimiwa Gavana kwa kutumia pesa za wananchi wa Mombasa ili kuweza kuwafanyia maendeleo katika siku zijazo.

Mheshimiwa Spika vile vile napenda kuunga mkono kwa sababu kadha, ndani ya wadi ya Bamburi nina imani na ninajua ya kwamba katika fedha hizi kuna kituo cha kuzima moto Kiembeni ambayo ilikua ikijengwa kila mwaka ikiwekewa fedha na najua ya kwamba katika *Supplementary Budget* hii kituo cha kuzima moto cha Kiembeni kimewekewa hela ili iweze kujengwa kumaliziwa, vile vile kuna sehemu ya Kimbunga ambayo najua imewekewa fedha katika *Supplementary* hii ili wapelekewe maji yatoke katika sehemu ya Kimbunga ipitie kwa jirani yangu hapa wadi ya Mwakirunge, Marimani ikishuka kwa wananchi wangu wa Mdengerekeni; vile vile najua katika *Supplementary Budget* hii wananchi wangu ambao wanahitaji kutengenezewa barabara haswa kule Bombo kuunganisha kipande kidogo kilichobaki najua pia kwamba nao wameweza kuwekewa. Kikubwa vile vile ni kuwaambia wananchi ama waheshimiwa ya kwamba kuna mradi unaitwa NAFSDP ambayo vile vile tulikuwa tunafaa tuwe tunapata *counter funding* kama County na katika *Supplementary* hii katika Idara yetu ya Kilimo *counter funding* ya mradi huo imewekwa ilmuradi wa NAFS DP uweze kuanza kuweza kuwafaidisha wakulima wetu na pia vile vile vijana ambao wangetaka kuinga maswala ya ukulima. Mwishowe Mheshimiwa Spika ni kuomba serikali yetu ya Kaunti upande wa utawala pesa hizi si kama Assembly jukumu letu ni kupitisha sheria na moja wapo ya sheria ni hii *Supplementary Budget*, tumepitisha sheria tunachotaka ni kwamba iweze kutekelezwa ili wananchi wetu waweze kufaidika na sisi nasi pia twaweza kuonekana tunafanya kazi na wananchi wetu waweze kua na imani zaidi ya kutuma viongozi wao waje kuwafanyia kazi kama hii; kwa hivyo nasema ahsante na Mwenyezi Mungu atubariki sote na abariki utenda kazi utakao kua uko mbele kupitia *Supplementary Budget* hii. Ahsanteni.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Patrick Mbelle. Yes, Honourable Amriya Juma Boy?

Hon. Amriya Juma: Thank you Mr. Speaker. I also rise to welcome The Kigwede Girls Secondary School and to advise them that this is an opportunity for them to learn the roles of the County Assembly as enshrined in the Constitution and Article 176, 177, on the roles of County Assembly that is making laws and plans, having oversight over the County Government and making budgets just like today we are having the supplementary budget and also the supplementary budget is also anchored in the Constitution, I think under Article 223 or something and also the PFM Act so this gives the girls an opportunity to experience first-hand education when you come to the Parliament Buildings. You are experiencing the debates first-hand. You are experiencing how the Members of the County Assembly famously known as MCAs how they enact laws and pass budgets, just like today and I hope this opportunity will enable you to go back to your books and read hard and become very prominent advocates, teachers, scientists, nurses. We have all cadres of professions in this House so feel encouraged today as you go back to your books, feel encouraged that you have seen great men and women here at the County Assembly that are doing exceedingly well and tremendously good work; so, with that much said I also rise to support the second reading of the Mombasa County Appropriation Bill as presented by the Chairman of Finance. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you, Honourable Amriya Boy Juma Boy she is the daughter of the late Kwale, not Kwale Senator, the former MP of Lunga Lunga and later he became the Senator of Kwale County. Thank you, Majority Leader for the Rectification. Yes, Honourable Nusura Mwinyi?

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kuniona ili na mimi nichangie. Kwanza nataka niwakaribishe sana wanafunzi kutoka shule ya upili kule Kingwede na pia kuchagua kuja ndani ya Bunge la Mombasa Kaunti kuja kusoma yale ambayo tunayoyafanya hapa ndani ya Bunge karibuni sana. Pili, nataka niseme nauunga mkono hoja hii iliyoletwa hapa Bungeni, kwanza niseme tumekaa kwa muda na sisi watu ambao tumechaguliwa kule na wananchi na wananchi wanatuangalia kwa kua wametuchagua kutuleta hapa wakingoja matunda ambayo tutayatoa hapa tuyapeleke kule mashinani. Mimi nimesimama hapa mwakilishi wadi wa Mtongwe wadi ambaye nilitumwa na watu wa Mtongwe wadi ambayo nilitumwa na watu wa Mtongwe na juzi nilikuwa kwa kikao cha watu wangu wa Bububu ambao iko Mtongwe wakiwa na malalamiko mengi sana kuhusu Barabara za Bububu kwa sababu ni mji mpya, lakini kwa kuwa leo hii tuko hapa na tutaenda kupitisha hii hoja ya bajeti najua watu wangu wa Mtongwe watakata Barabara ambazo saa hii hakupitiki hakwendeki na mvua ikizidi kunyesha naona wengine watakuwa wanalala mjini, kwa maana hiyo nimesimama kuunga mkono Mheshimiwa spika. Ahsante Sana.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Athman Mwamwiri Majority Leader.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Ahsante sana Mheshimiwa spika niungane na wenzangu kuunga mkono hoja hii, lakini kuweka taarifa sawa isije wanafunzi wa Kigwede wasije sema hatukuwatendea haki, Mheshimiwa Boi alikuwa Mbunge wa Matuga sio Lunga Lunga kisha baadae ndio akaja akachaguliwa kama Seneta wa jimbo la Kwale. Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa katiba ibara 223 kama alivyonukuu Mheshimiwa wakili imepeana ruksa ya

kwamba serikali ziweze kuitengeza bajeti ya nyongeza ama bajeti ya ziada. Kw lugha ya kimombo yaitwa supplementary kwa hivyo Mheshimiwa Spika zoezi hili ambalo Mwenyekiti anaazimia kulitekeleza lipo kwa mujibu wa sheria katiba ya Jamhuri yetu ya Kenya, vile vile Mheshimiwa Spika unaposoma ilani ya 35 ya 2015 ya usimamizi wa pesa za ummah ya serikali za Ugatuzi ili kwenye kunukuu watataka kupitia Public Finance Management County Government Regulations number 35 of 2015. Sehemu ya 39 Sehemu ndogo ya tatu inazungumzia shabaha ya bajeti ya nyongeza Mheshimiwa Spika na sababu kuu ya kutengenezwa bajeti hii, moja Mheshimiwa Spika ni kwa sababu ndani ya bajeti inapotengezwa baada ya mda hubainika ya kwamba kuna fedha ambazo hazitaweza kutumika katika mwaka ule wa kifedha. Pili, Mheshimiwa Spika kuna sababu nyengine ambayo huchangia kutengezwa kwa bajeti ya ziada ya kwamba katika bajeti kuu iliyotengezwa huenda ikawa kuna pesa zilikadiriwa kwa mradi ambao pesa zile hazitaweza kupatikana kutekeleza mradi ule, Mheshimiwa Spika vile vile pia hutokea katika bajeti kuu ikawa kuna kasoro ama kuna uwezekano wa kutokufikia kiwango cha pesa zilizo tarajiwa katika bajeti kuu iliyo pitishwa, kulingana mda ulio tekelezwa.

Hivyo basi sheria kwa mujibu wa katiba na ilani hii imeruhusu ya kwamba serikali chini ya idhini tunaweza kufanya bajeti ya ziada Mheshimiwa Spika kuweka mambo sawa kwa kuzingatia mambo matatu haya ya fedha ambazo haziwezi kutumiwa fedha ambazo hatutaweza kuzipata na vilevile kasoro ambazo ziko katika bajeti kuu, Mheshimiwa Spika kwa sababu watekelezaji ama watawala wanapewa ruksa ya kuweza kufanya marekebisho bajeti yasiozidi asilimia kumi lakini chochote kinachozidi asilimia kumi ni lazima yaweze kupitishwa kwa mujibu na idhini ya Bunge kama tulivyo hapa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nisihi tu Waheshimiwa wenza na kama walivyo onyesha nia njema ya kwamba tuweze kusimama kuunga mkono hoja hii kuendelea na zoezi la kutengeza bajeti ya ziada ili hii kuiwezesha serikali kwa upande wa utawala kutekeleza maazimio na malengo sisi kama wakilishi imekuwa ni vilio vya wananchi wetu kule Mashinani, naunga mkono. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Athman Mwamwiri. Yes, Honourable Kibwana Baya please reply to your Motion?

Hon. Kibwana Swaleh: Thank you Mr. Speaker, I am happy that most of the members have supported this Motion, Honourable Speaker I want just to highlight some few issues for regarding this supplementary budget for the first time as an Assembly and as a county government we are going to do a one-kilometre road to three sub counties that is Jomvu, Likoni and Kisauni Honourable Speaker it is my view that as a Chair and also with my members including the Executive we are going to discuss the next financial year that we will be able to carry the other three sub counties in terms of road that is one kilometre road. Honourable Speaker, you are aware that we have bursary that have not been given the money to the schools, the boarding school in this supplementary budget on the Speaker, the County Government has allocated Ksh.250Million so that we are able to pay a bursary for the boarding school...

[Applause]

Honourable Speaker, you aware that also we have passed revolving fund in this supplementary budget, there is Ksh.100 Million that are going to be allocated to a group that is youth and women Honourable Speaker. Honourable Speaker, we also have a *Kamukunji* yesterday with the Members and we are able to allocate....

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Kibwana do not discuss your *Kamukunji* in this Honourable House.

Hon. Kibwana Swaleh: Thank you Honourable Speaker for your guidance. We have allocated Ksh.2 Million per Ward that is for driving for our youth Honourable Speaker. So, Honourable Speaker you will find in this supplementary budget there are some Wards that have not been touched in terms of development Honourable Speaker. I am aware of that; I want to assure Members that when we come to the next financial year, that is 2026/2027 the Wards that have not been getting a mega project we will be able to allocate. So, mine is just to appreciate that this supplementary budget will make us move as a County and also, we will be able to see some development in our Wards Honourable Speaker. With those few remarks Honourable Speaker, I really appreciate your office as well as my Committee including my Vice Chair and Members and also my colleagues and also the secretariat for making a good job. Thank you, Honourable Speaker.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Members. I now put the question that the Motion by the Members of the Committee on Finance, Budget, and Appropriation for the Mombasa County Supplementary Appropriation Bill, 2026 to be read a second time.

[Question put and agreed to]

Yes, Clerk. Please read the bill for the second time.

[The Bill was read for the second time]

Yes, Clerk.

ADJOURNMENT

Honourable Members, there being no other business, the House stands adjourned until Wednesday, 11th March, 2026 at 10:00a.m.

The House rose at 3:12p.m.